**HOTUBA YA MHESHIMIWA DKT. SAMIA SULUHU HASSAN, RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, KATIKA MAZISHI YA KITAIFA YA HAYATI ALI HASSAN MWINYI, RAIS MSTAAFU WA AWAMU YA PILI WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, ZANZIBAR, TAREHE 02 MACHI, 2024**

- *Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi;*
- *Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;*
- *Mheshimiwa Netumbo Nandi-Ndaitwah, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Namibia;*
- *Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri wa Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;*
- *Mheshimiwa Othman Masoud Othman, Makamu wa Kwanza wa Rais – Serikali ya Mapinduzi Zanzibar,*

- *Mheshimiwa Hemed Abdulla, Makamu wa Pili wa Rais – Serikali ya Mapinduzi Zanzibar;*
- *Waheshimiwa Viongozi Wakuu Wastaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar;*
- *Makamu Mwenyekiti, Katibu Mkuu na Uongozi wa Kitaifa wa Chama cha Mapinduzi;*
- *Viongozi wa Kitaifa wa vyama vingine vya kisiasa;*
- *Mhe. Zubeir Ali Maulid, Spika wa Zanzibar;*
- *Mheshimiwa Mussa Azan Zungu (Mb), Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;*
- *Mheshimiwa Emmanuel Sinzohagera, Spika wa Bunge la Seneti la Burundi;*
- *Mheshimiwa Prof. Ibrahim Juma, Jaji Mkuu wa Tanzania;*
- *Mheshimiwa Khamis Ramadhan Abdalla, Jaji Mkuu wa Zanzibar;*

- *Mama Sitti Mwinyi na Mama Khadija Mwinyi, Wajane wa Marehemu pamoja na Familia na Ndugu wote wa Marehemu;*
- *Wenza wa Viongozi;*
- *Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri mliopo;*
- *Mheshimiwa Humoud Msaidie, Waziri wa Kilimo wa Umoja wa Visiwa vya Komoro;*
- *Waheshimiwa Wabunge na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi;*
- *Makatibu Wakuu Viongozi;*
- *Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu;*
- *Waheshimiwa Mabalozi wanaowakilisha Nchi mbalimbali na wawakilishi wa Mashirika ya Kimataifa wakiongozwa na Amidi Mheshimiwa Ahamada El Badaoui;*
- *Wakuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama;*
- *Waheshimiwa Viongozi wa Vyama mbalimbali vya Siasa;*

- ***Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya;***
- ***Waheshimiwa Viongozi wa Dini;***
- ***Ndugu viongozi mbalimbali wa Serikali;***
- ***Waandishi wa Habari;***
- ***Mabibi na Mabwana.***

***Assalaam Aleykum***

**Ndugu zangu,** tumekusanyika hapa leo kutoa heshima zetu za mwisho na kumuaga kiongozi wetu mpendwa mwenye historia kubwa na nchi yetu, Jumuiya yetu ya Afrika Mashariki na Bara la Afrika kwa ujumla. Mzee wetu, Alhaj Ali Hassan Mwinyi aliipenda nchi yake Tanzania, na aliitumikia kwa moyo wake wote. Aliingoza nchi yetu na kuivusha katika vipindi vigumu, kwanza akiwa Rais wa

Zanzibar na baadaye kama Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Ingawa tuna simanzi na masikitiko ya kuondokewa na moja ya nguzo imara za taifa hili, ila faraja yetu ni kwamba tumeweza kumuenzi kwa kumpa maziko ya Kitaifa na kumuombea dua njema. Ni jambo analostahili kwa namna alivyolipambania Taifa hili. Kifo chake ni pigo kwa Taifa, na kwangu binafsi kama Mkuu wa Nchi. Nimeukumbuka msemo wa Kiafrika usemao, ***anapofariki mzee, maktaba huungua moto.*** Pia tunaambiwa kuwa CV (*wasifu*) hairithiwi. Mtakubaliana nami kwamba, maktaba yetu moja kubwa iliyosheheni hadithi nyingi na nzuri imeungua moto. Mzee Mwinyi alikuwa ni maktaba inayotembea na

iliyosheheni vitabu vyenye mafunzo ya uadilifu, uzalendo ustahimilivu, mageuzi, ujasiri, unyenyekevu na uchamungu miongoni mwa mafunzo mengi mengine.

Kwa kuwa tunayasadiki maneno ya Qur'an Tukufu kwenye **Surat Al-Anqabut, aya ya 57**, yasemayo, ***kila nafsi itaonja mauti, na kwake tutarejea*** pamoja na majonzi na simanzi tuliyonayo hatuna budi kupokea mapenzi yake Mungu kwa unyenyekevu na subra. **Inna lillahi wa inna ilayhi raji'un**

***Ndugu zangu,***

Japo msiba huu ni wa kitaifa, ni wetu, ila ni msiba mkubwa zaidi kwa familia kwa kuondokewa na nguzo yao na mpendwa wao. Juzi nilishiriki mazishi ya aliyekuwa

Rais wa Hage Geingob, Hage Geingob, kila mara walikuwa wanasema 'Mbuyu wetu umeanguka.' Na kwetu sisi, Mbuyu umeanguka.

Kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ninatoa pole kwa mama zangu, Sitti Mwinyi na Khadija Mwinyi, watoto wa marehemu wakiongozwa na Mheshimiwa Rais Dkt. Hussein Ali Mwinyi, wajukuu na vitukuu, kwa kuondokewa na mmoja kati yao. Tambueni kuwa pigo hili ni pigo letu na kamwe hamko pekee yenu, tuko pamoja nanyi .

Sote tunafahamu ni kwa namna gani Ulamaa Alhaj Ali Hassan Mwinyi alivyokuwa mchamungu alieijua, kuishika, kuyaishi kuyathamini na kuyaenzi mafunzo ya dini yake ya

Kiislam. Pamoja na hayo, kama alivyokuwa anapenda kusema yeye mwenyewe, *'lisilo budi hutendwa'*. Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi aliwahi kuwa Kiongozi wetu wa Kitaifa, akiwa mtu pekee kuwahi kushika nafasi ya Rais wa Tanzania na Rais wa Zanzibar. Hivyo, ilikuwa lazima wananchi wa Tanzania na wakazi wa Zanzibar wapate nafasi ya kumuaga Kiongozi wao huyu wa Kitaifa. Ndio maana kufuatia mashauriano baina ya familia na Serikali, tunashukuru kwamba tumeweza kumpatia mpendwa wetu heshima zote kama Rais Mstaafu wa Tanzania na Rais Mstaafu wa Zanzibar.

Nitumie fursa hii sasa kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Kassim Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri

ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Hemed Abdulla, Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar pamoja na Kamati ya Mazishi ya Kitaifa kwa uratibu mzuri wa shughuli hii ya Kitaifa, licha ya muda mfupi wa maandalizi. Niungane nanyi pia kuvishukuru pia Vyombo vya Ulinzi na Usalama kwa kuhakikisha kuwa tunaweza kukamilisha zoezi hili.

Aidha, niwashukuru viongozi wa dini, na wananchi mbalimbali kwa dua na sala zenu tangu mpendwa Rais wetu alipokuwa hospitali hadi leo tunapompumzisha kwa heshima zote za kitaifa. Kipekee niungane na Ndugu Abdullah Mwinyi niwashukuru madkatari na wahudumu wetu wa afya wote waliokuwa wanamhudumia Mzee wetu

kipindi chote cha ugonjwa mpaka umauti kumfika. Kwa waombolezaji wenzangu kwanza tuwe pole na Niwashukuru kwa kujitokeza kwa wingi pale Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam na leo hapa Uwanja wa Amaan, Zanzibar kumuaga kwa heshima aliyostahili.

Nitumie fursa pia kuwashukuru Viongozi kutoka nchi za kigeni ambao wametuma salamu za pole na rambirambi kwa Serikali na Watu wa Tanzania kufuatia msiba huu. Kwa heshima kubwa na unyenyekevu niwashukuru nchi rafiki zilizotuma wawakilishi wake ndani ya muda mfupi tangu tutangaze msiba na maziko. Tupo na ndugu yetu Mheshimiwa Netumbo Nandi-Ndaitwah, Makamu wa Rais wa Namibia, Spika wa Bunge la Seneti la Burundi na Waziri

wa Kilimo kutoka Komoro. Wakati tunaingia hapa mlituona mimi na Rais Mwinyi tukiongea na simu tukipokea salaam kutoka kwa Marais kadhaa wa nchi jirani wakitupa pole. Tunawashukuru wote.

***Baadhi ya masuala ya kihistoria***

***Ndugu zangu,***

Mapito ya Mzee Mwinyi yana mafunzo na historia mbalimbali za kipekee. Zaidi ya Hayati Mwinyi, kuwa yeye ndiye Mtanzania wa Kwanza kuwahi kuwa Rais wa Zanzibar na baadaye Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alikuwa kiongozi katika vipindi vigumu kisiasa na kiuchumi. Rais Mwinyi aliweza kuhakikisha utulivu na

kufanya mageuzi makubwa katika nyanja za kisiasa, kijamii na kiuchumi Zanzibar na Tanzania Bara.

Hayati Mwinyi, pia alikuwa ni Rais wa Kwanza kuiongoza Tanzania mara baada ya mabadiliko ya Katiba kufanyika mwaka 1984 yaliyojumuisha Haki za Binadamu (Bill of Rights) kwenye Katiba. Wakati wa uongozi wake, licha ya kwamba nchi yetu haikuwa na uzoefu wa kusikia sauti kinzani, nchi yetu ilikuwa na Chama kimoja, lakini kwa hulka yake ya ustahimilivu, aliweza kuliongoza jahazi la Tanzania inayoheshimu haki za binadamu na utawala bora na kuruhusu maoni tofauti na yale yaliyozoeleka kwa maana Serikali. Aliruhusu magazeti ya watu binafsi, vituo vya redio pamoja na vituo vya televisheni vilipata fursa, na

pia asasi mbalimbali za kiraia zilipata pia fursa ya kupaza sauti na kuikosoa Serikali. Mzee Mwinyi aliweza kuhimili sauti mbadala na aliweza kulivusha Taifa.

Mzee Mwinyi pia ndiye aliyesimamia mageuzi ya kisiasa na kufanikiwa kurejesha mfumo wa vyama vingi nchini mnamo mwaka 1992 baada ya kufutwa mwaka 1965. Na hivyo Mzee Mwinyi kujipatia jina rasmi kama Baba wa Demokrasia nchini.

Pamoja na kuwa kiongozi wa kitaifa, Rais Mwinyi pia alikuwa kiongozi ndani ya Chama cha Mapinduzi, na alituongoza vyema kwenye Chama.

Mzee Mwinyi ndiye aliyeruhusu uwekezaji kutoka sekta binafsi au kampuni binafsi, na kwa mara ya kwanza

makampuni binafsi ya simu yaliweza kuwekeza Tanzania. Ninakumbuka kampuni za kwanza zilikuwa zinaitwa Mobitel, zile zenye *antenna*. Na kwa maana hiyo simu zote zilizofuata tuliziita Mobitel kabla ya kujua na kuziita majina yake halisi.

Hizi ni baadhi tu ya alama za kudumu za kihistoria zilizoachwa na Mzee Mwinyi. Alama hizo ulizisaidia Serikali za awamu zote zilizofuatia. Kwa mfano, kuhamasisha sekta binafsi na soko huria, Serikali ya Mzee Mkapa ilipata pa kuanzia katika suala la ukusanyaji mapato. Vivyo hivyo kwa majadiliano na Shirika la Fedha Ulimwenguni na Benki ya Dunia na mengineyo, Serikali ya

Mzee Mkapa ilipata pa kuanzia wakati wa majadiliano ya kufutiwa madeni ya wahisani.

### *Masuala atakayokumbukwa kwayo*

**Ndugu zangu,** kwa upande wa mafunzo kutokana na maisha ya Mzee Mwinyi, mengi yamekwishasemwa hapa na hata kabla ya leo. Mengine pia yataendelea kusemwa. Kwa muktadha wa hotuba yangu, ninaomba mridhie nigusie mafunzo machache tu ambayo tunayapata kutokana na hadithi ya maisha ya Mzee Mwinyi.

### Uanamageuzi usioyumba

Moja ya sifa kubwa tunayoipata kupitia maisha ya Mzee Mwinyi ni kuwa alikuwa mwanamageuzi shupavu na asiyeyumba. Hadi mwaka 1985 Serikali yake ilikuwa

haijakubaliana na masharti magumu na sera mpya za kiuchumi zilizotangazwa na Benki ya Dunia na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF). Kwa maana hiyo Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere aliamua kung'atuka ili kutoa fursa kwa mageuzi kuendelea kwa wale watakaoona kuna haja ya kuendelea na mageuzi.

Hivyo, Mzee Mwinyi alipokea uongozi wa Jamhuri yetu, nchi yetu ikiwa uchumi dhaifu, uchache wa fedha za kigeni, nchi wahisani zilisitisha misaada ya bajeti, na mapato ya ndani nayo yalikuwa haba. Mambo haya yalipelekea kuadimika kwa bidhaa muhimu madukani, hali iliyoleta kero kwa wananchi.

Mabadiliko yalikuwa ni lazima, lakini mazoea nayo yaliwatatiza wananchi na Chama. Tatizo lilijulikana, jawabu lilifahamika, lakini ndani na nje ya nchi hakuna aliyeamini kuwa mabadiliko yangewezekana kutekelezwa bila kuyumbishwa. Kwa mfano, jarida la masuala ya kiuchumi la Uingereza *The Economist* liliandika, naomba kununukuu ***"Dont expect many changes in Tanzania's lackluster economy when Ali Hassan takes over as President....Mr. Mwinyi is Nyerere's man."*** Yaani, 'msitarajie mabadiliko mengi katika uchumi dhaifu wa Tanzania kwa Ali Hassan Mwinyi kuwa Rais, kwani Mwinyi ni kijana wa Nyerere'. Waliandika haya bila kutanabahi kwamba Mwalimu Nyerere aling'atuka kutoa nafasi kwa mageuzi, na Mzee Mwinyi alichukua nafasi hiyo kufanya mageuzi.

Kinyume na utabiri huo, kama Mzee wetu alivyowahi kusema kwamba kila zama na kitabu chake, baada ya kushauriwa vizuri na wataalam, ikiwemo aliyekuwa Waziri wake wa Fedha, Mzee Cleopa David Msuya, Rais Mwinyi aliridhia kuendelea na mazungumzo na Benki ya Dunia na Shirika la Fedha Duniani.

Mzee Mwinyi aliwahi kutuambia kwamba dawa ya IMF ni chungu sana, lakini kwa maradhi yanayouma uchumi wetu, ni lazima tuinywe. Tulinywa dawa ile, na nchi iliingia kwenye mfumo wa soko huria. Pamoja na mambo mengine, hii ilikuwa ni tiba ya ule mkwamo wa

muda mrefu wa ukosefu wa bidhaa muhimu madukani. Na hapa ndipo alipojipatia jina maarufu ya Mzee Ruksa.

Kama mnavyoona, hata sasa, tunaendelea kunufaika na uamuzi wa kuruhusu soko huria.

### *Kuishi kwa kufuata misingi bora*

Suala lingine ninalotaka kulisema ni kuwa, Mzee Mwinyi aliishi kwa kufuata misingi bora ya maisha katika uhai wake wote.

Ninakumbuka siku moja tukiwa kwenye matembezi ya hiari, kwenye kampeni ya *Afya Yangu, Mtaji wangu,* tuliongozwa na Mzee Mwinyi. Na mara zote alikuwa anaongoza alafu anakwenda mbele na kunisubiri, akiuliza 'Mama uko wapi', na ninaenda, ninamfuata. Tunaanza

kwenda na baada ya muda amenipita tena. Lakini tulipofika viwanja vya *Leaders Club* kufanya mkutano, ninakumbuka waandishi wa habari waliomba kumhoji. Moja ya maswali walilomuuliza ni Mzee na umri wako umeweza kutembea kama kijana wa miaka 40, siri ni nini. Aliposimama Mzee Mwinyi akasema kwanza siri ni kufanya mazoezi, lakini kwa wale vijana wa kiume wanifuate pembeni nije niwaambie siri ni nini. Kwa hiyo ina maana aliishi na mwongozo maalum katika maisha yake.

Kama inavyohadhithiwa, kwamba Baba yake alitamani mwanaye asome elimu ya dini ili awe Sheikh Mkubwa katika ukanda huu. Ingawa ndoto hii, Mzee

Mwinyi alitambulika kama mmoja wa wanazuoni wazuri na Mzee wa Twariq.

Katika simulizi kuhusu maisha yake, Mzee Mwinyi alieleza kuwa akiwa kijana Baba yake alimsihi kuwa 'mchamungu, mnyenyekevu, asiyejiona bora kuliko wengine, mtumishi wa watu kwa shida zao, mkarimu, na mtu asiyekata shauri pekee yake juu ya masuala muhimu.'

Mafunzo ya dini pamoja na nasaha za Baba yake yaliendelea kuwa msingi mzuri na nguzo imara katika maisha na uongozi wake. Hekima hii aliyoipata kwa Mzee wake inaweza kuwa ndio chachu kukubali kuendelea kuwa Mlezi wa Chama cha Skauti Nchini hata akiwa na umri mkubwa wa miaka 94. Aliamini bado ana jukumu la

kutumia uzoefu wake na karama yake ya uongozi kulea vijana wengi zaidi. Nikiwa ninamkabidhi ulezi wa Chama cha Skauti ndipo alipoacha wosia wa kuwa maisha ni hadithi, na ni vyema mtu ukaandika hadithi nzuri kwa wale wakaosimulia hadithi yako. Akiwa anawasihi viongozi wa Skauti kutenda mema na kutomtia aibu kwamba yeye ndio alikuwa mlezi wao.

Hii inatukumbusha nafasi muhimu ya malezi na kuweka misingi bora itakayotuongoza katika maisha yetu yote. Maisha ya Mzee Mwinyi yawe funzo kwa familia zetu katika kuwalea vijana wetu katika maadili ya dini na hofu ya Mwenyezi Mungu.

Jambo jingine tunaloweza kujifunza ni kwamba, ingawa kuna misingi inayowekwa tukiwa vijana, yapo mambo mengine mema unaweza kujifunza ukubwani. Mzee Mwinyi akiwa na umri wa miaka 90, alipata kusema kwamba, tangu akiwa na umri wa miaka 50, amekuwa akifanya mazoezi yanayohusisha kutembea kilomita 5 kwa siku, na aliongeza kwa kusema anaendesha baiskeli kwa nusu saa jioni. Alisema hivyo ili kuwatia ari wananchi kufanya mazoezi kwa kuwa ni njia ya kulinda afya na kujiepusha na magonjwa yasiyokuambukizwa kama vile kisukari na presha. Ni matumaini yangu, sote tutajifunza kitu kuhusu mazoezi. Kwamba, hata ukiwa na umri mkubwa wa miaka 50, bado hujachelewa kuweka misingi bora ya maisha. Kikubwa ni kuanza, na kuwa na nidhamu

ya kuendelea. Nadhani hapa Profesa Janabi ameweza kuendeleza wosia huu vizuri, na hatuna budi kumsikiliza na sio kumbeza.

**Uongozi wa kuwajibika**

***Ndugu Wananchi,***

Miaka 48 iliyopita, Mzee Mwinyi, alitupa funzo kubwa kuhusu utayari wa kiongozi kuwajibika. Ninapenda kunukuu sehemu ya maneno yake kwenye barua ya kujiuzulu Uwaziri ***"Kisiasa nakiri kuwa nahusika, siwezi kukwepa kwa sababu dhamana yangu ya uwaziri inaambatana na wajibu unaonitaka nijue yanayotendeka Wizarani na pia niweze kudhibiti na kuhakikisha mwenendo mwema wa Jeshi la Polisi"***. Ameonesha

kwamba cheo ni dhamana, kwamba lililotendeka ni dhamana yake. Tujiangalie tuliopo Mawizarani sasa, kama tunahabari na yanayotendeka, na kama tunawajibika kwa hayo yanayotendeka. Lakini aliona ni jambo la heshima kwake, kwamba aweke historia na rekodi kwa Serikali na kwa Chama chake, kwamba kiongozi unapoongoza mahali panapokosewa ni lazima uwajibike. Sasa tujipime nasi, cheo ni dhamana, tunatumia vipi dhamana zetu.

Aidha, alivyokuwa Rais alisisitiza kuwa kazi ya kusimamia uwajibikaji 'ni ya kudumu na inaweza kufanywa kwa ufanisi mkubwa bila matangazo au vishindo, kwani wananchi wanachotaka kuona ni kutoweka kwa uzembe, wizi na ubadhirifu na siyo kuorodhesha

maovu ambayo tayari wanayajua'. Hatuna budi kumuenzi mzee wetu kwa kuiishi dhana ya uwajibikaji kwa mapana hayo.

### *Nitakavyomkumbuka*

Mzee Mwinyi alikuwa ni mzee wangu. Nitamkumbuka kwa uzalendo wake, uchamungu wake, na hekima zake. Nitamkumbuka pia kwa mapenzi yake kwa lugha yetu adhimu ya Kiswahili na kujitolea kwake kwenye shughuli za kijamii. Afrika Mashariki itamkubuka kwa kuwa moja wa waasisi wa kufufuliwa kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki; Afrika kwa ujumla itamkumbuka kwa kusimamia kukamilisha jitihada za ukombozi Kusini mwa Afrika zilizohitimishwa na ukombozi wa Jamhuri ya Afrika

Kusini mwaka 1994. Mzee Mwinyi pia atakumbukwa kwa mchango wake katika kutoa hifadhi kwa wakimbizi waliokimbia vita katika Ukanda wa Maziwa Makuu na kuchangia jitihada za kutafuta amani na utulivu wa ukanda huo.

Mimi binafsi nitamkumbuka. Katika hatua za mapito yangu ya uongozi wa nchi hii, nilikuwa najaribu sana kuchota hekima kwa Mzee Mwinyi na kufuata mapito yake. Lakini sidhani kama nimeweza kuvaa viatu vyake. Ninachoweza kusema ni hasara kwamba sasa maktaba imeungua. Ninakumbuka wakati tunaadhimisha kuzaliwa kwake, nilimuomba Mwenyezi Mungu amjalie Mzee Mwinyi afike miaka 100, na nikijua atafika miaka 100 akiwa

mzima vilevile. Nitampigia simu kumwambia ‘Mzee ninakuja kukuona’, na yeye atasema ‘njoo mwanangu.’ Ukifika anachekesha, anakupa mawaidha, anakupa hekima, anakupa busara, unachota kwenye kisima chake cha hekima. Lakini ukipanga yenu, Mungu anapanga yake. Sote ni waja wake, na kwake tutarejea. Ninaloweza kusema ni kwamba maktaba yangu imeungua.

Ahadi yangu ni kwamba, nitaendelea kuyaenzi na kuyaishi maono yake, kwa kusimamia ustawi wa wananchi, kushamirisha sekta binafsi, kutenda haki na kuwa na subra na ustahimilivu.

Niseme tu, Mzee Mwinyi alikuwa ni hidaya kwa Watanzania. Alitabiriwa makubwa na baba yake mzazi kwa

kumuita jina *Nzasa*, kumaanisha **mtu asiyekaukiwa**. Na kwa kweli Mzee Mwinyi hakukaukiwa na hekima, busara na wingi wa uchamungu. Hakika kwa mafunzo haya katuacha sadaka ya Elimu na yeye Allah atamlipa kwa sadaka hii, Amin.

Kwa ndugu zangu, Dr. Hussein, Abbas, Mohamed, Abdullah, Amour, Asha, Fatma, Juma, Salama, Halima na Asri, pia kwa Mama zetu Mama Sitti na Mama Khadija, kwa ndugu jamaa na marafiki, ***mbuyu umeng'oka.*** Niwasihi na kuwaomba kuimarisha udugu na mshikamano kwa ukoo wa Mwinyi, kuendelea kutunza heshima ya Mzee wetu. Na mbuyu unapong'oka, si shida kupata mwingine. Kati yenu kumi na moja mliyebaki, moja asimame awe

mbuyu wa ukoo huu. Hatutafurahi kusikia kuwa familia ina migogoro au inatatizana. Hapa nikusihi sana Dr Hussein simama kuwa mbuyu wa familia.

**Inna Lillahi, Wainna Illeihi Rrajiuun!**

**Hakika wote ni wa Mwenyezi Mungu, na kwake tutarejea.**

**Ahsanteni sana kwa kunisikiliza.**